# Mistari ya biblia kuhusu watoto

---

Jiunge na group la Whatsapp, ujifunze biblia na upate Neno la siku kila asubuhi. kwa link hii >>> https://chat.whatsapp.com/GRri9BATojl2FNGbOJpjC6

Tazama mistari hii, na chini kabisa utapata orodha ya masomo ya kujifunza kuhusu watoto, kwako wewe kama mzazi/mlezi.

> *Isaya 54:13 “Na watoto wako wote watafundishwa na Bwana; na amani ya watoto wako itakuwa nyingi”.*

> *Mathayo 19:14 “Lakini Yesu akasema, Waacheni watoto*

*wadogo waje kwangu; wala msiwazuie; kwa maana walio mfano wa hao, ufalme wa mbinguni ni wao".*

*Wakolosai 3:20 "Ninyi watoto, watiini wazazi wenu katika mambo yote; maana jambo hili lapendeza katika Bwana".*

*Mithali 1:8 "Mwanangu, yasikilize mafundisho ya baba yako, Wala usiiache sheria ya mama yako,*

*9 Kwa maana hayo yatakuwa kilemba cha neema kichwani pako, Na mikufu shingoni mwako".*

*Waefeso 6:1 "Enyi watoto, watiini wazazi wenu katika Bwana, maana hii ndiyo haki.*

*2 Waheshimu baba yako na mama yako; amri hii ndiyo amri ya kwanza yenye ahadi,*

> *3 Upate heri, ukae siku nyingi katika dunia”.*

> *Luka 2:52 “Naye Yesu akazidi kuendelea katika hekima na kimo, akimpendeza Mungu na wanadamu”.*

> *3Yohana 1:4 “Sina furaha iliyo kuu kuliko hii, kusikia ya kwamba watoto wangu wanakwenda katika kweli”.*

> *Marko 10:15 “Amin, nawaambieni, Ye yote asiyeukubali ufalme wa Mungu kama mtoto mdogo hatauingia kabisa.*
>
> *16 Akawakumbatia, akaweka mikono yake juu yao, akawabarikia”.*

> *1Timotheo 4:12 “Mtu awaye yote asiudharau ujana wako, bali uwe kielelezo kwao waaminio, katika usemi na*

*mwenendo, na katika upendo na imani na usafi".*

*Zaburi 127:3 "Tazama, wana ndio urithi wa Bwana, Uzao wa tumbo ni thawabu".*

*Zaburi 34:11 "Njoni, enyi wana, mnisikilize, Nami nitawafundisha kumcha Bwana".*

*Mithali 22:6 "Mlee mtoto katika njia impasayo, Naye hataiacha, hata atakapokuwa mzee".*

*Mithali 22:15 "Ujinga umefungwa ndani ya moyo wa mtoto; Lakini fimbo ya adhabu itaufukuzia mbali".*

*Mithali 23:13 “Usimnyime mtoto wako mapigo; Maana ukimpiga kwa fimbo hatakufa.*

*14 Utampiga kwa fimbo, Na kumwokoa nafsi yake na Kuzimu”.*

*Mithali 13:24 “Yeye asiyetumia fimbo yake humchukia mwanawe; Bali yeye ampendaye humrudi mapema”.*

*Mithali 19:18 “Mrudi mwanao, kwa maana liko tumaini; Wala usiikaze nafsi yako kwa kuangamia kwake”.*

*Waebrania 12:11 “Kila adhabu wakati wake haionekani kuwa kitu cha furaha, bali cha huzuni; lakini baadaye huwaletea wao waliozoezwa nayo matunda ya haki yenye amani”.*

> *Mithali 29:17 "Mrudi mwanao naye atakustarehesha; Naam, atakufurahisha nafsi yako".*

> *Mithali 17:6 "Wana wa wana ndio taji ya wazee, Na utukufu wa watoto ni baba zao".*

> *Waefeso 6:4 "Nanyi, akina baba, msiwachokoze watoto wenu; bali waleeni katika adabu na maonyo ya Bwana".*

Mafundisho muhimu ya wazazi kwa watoto.

> *KILEMBA CHA NEEMA, JE! UMEMVIKA MWANAO?*

> *LENGO LA SHETANI KWA WATOTO WA KIZAZI HIKI.*

*MALEZI YA MTOTO MCHANGA.*

*SIKU YA UNYAKUO ITAKUKUTAJE?*

*MAPIGO YA VITASA SABA, NA SIKU YA BWANA.*

*MKUMBUKE MKE WA LUTU.*

Rudi Nyumbani:

Je! utapenda mafundisho ya Neno la Mungu ya kila siku yawe yanakufikia kwa njia ya whatsapp au email yako? Kama ndio, basi tutumie ujumbe kwenye namba hii +255789001312

Share on:
WhatsApp